

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



16 Urambo Street
S. L. P 6420,
11102 Ilala
ILALA-DAR ES SALAAM
Simu 022-2132954

JUNI 16, 2020

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**TAKUKURU MKOA WA ILALA YAWAFIKISHA MAHAKAMANI
WATUMISHI WAWILI KUTOKA OFISI YA MTHAMINI MKUU WA
SERIKALI**

NDUGU WANAHABARI.

Ninapenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana Wanahabari kwa ushirikiano ambao mmekuwa mkiutoa kwa TAKUKURU kila tunapowaalika ili kuzungumza nanyi. Karibuni sana ofisi za **TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA MKOA WA ILALA.**

NDUGU WANAHABARI.

Tumewaita leo ili kuutarifu umma kwamba Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Ilala leo Tarehe 16.06.2020 kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka inatarajia kuwafikisha mahakamani (Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu) watumishi wawili ambao ni **ADAM YUSUF ADAM** na **PETER ELIAS MREMA** ambao ni Wathamini kutoka ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kwa makosa mbalimbali ya rushwa.

Katika tuhuma hizi **Mshtakiwa wa kwanza ADAM YUSUF ADAM** anashtakiwa kwa kosa moja la Matumizi Mabaya ya Madaraka kinyume na kifungu cha 31 cha Sheria Ya Kuzuia Na Kupambana Na Rushwa Na. 11/2007. Maelezo ya kosa ni kwamba mnamo tarehe 20.06.2016 akitekeleza majukumu yake kama Mthamini, kwa makusudi alitumia madaraka yake vibaya kwa kuthibitisha (*Verifying and Approving*) taarifa ya uthamini

kwa ajili ya malipo ya fidia ya mradi wa Dar es Salaam Metropolitan Development Project (DMDP) kwa Manispaa ya Ilala na Kinondoni na kukiuka Kifungu cha 19(1) na (4) cha Sheria Ya Wapima (The Professional Surveyors (Registration) Act) Sura ya 270 Toleo la 2002 na kupelekea **PETER ELIAS MREMA** kupata malipo ya **Tshs. 46,618,000/=**.

Mshtakiwa wa pili . PETER ELIAS MREMA anashtakiwa kwa makosa matatu, kosa la kwanza na la pili ni Kutumia Nyaraka Kumdanganya Mwajiri kinyume na kifungu cha 22 cha Sheria Ya Kuzuia Na Kupambana Na Rushwa Na. 11/2007. Maelezo ya kosa ni kwamba mnamo tarehe 20.06.2016 aliwasilisha kwenye ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uthibitisho (**Verifying and Approving**) taarifa za uthamini za Juni 2016 na Juni 2014 kwaajili ya malipo ya fidia kwa mradi wa DMDP kwa wananchi wa Manispaa ya Ilala na Temeke huku akijua taarifa hizo ya uthamini zilikuwa na taarifa za uongo.

Kosa la tatu ni kufanya kazi kama Mpima (**Surveyor**) bila kusajiliwa na bodi ya wapima kwa mradi wa DMDP kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi wa Manispaa ya Temeke na Ilala wakati akijua wazi alikua hajasajiliwa kinyume na kifungu cha 19(1) na (4) cha Sheria ya Wapima (**The Professional Surveyors (Registration) Act**) Sura ya 270 Toleo la 2002.

NDUGU WANAHABARI,

Baada ya maelezo hayo napenda kuwashukuru tena wanahabari kwa ushirikiano wenu.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA

Imetolewa na:

Christopher Myava
Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Ilala